CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

IDARA YA SAYANSI YA SIASA NA UTAWALA

MPANGO WA UTAFITI NA ELIMU YA DEMOKRASIA TANZANIA (REDET)

REDET OPINION POLL

MAONI YA WANANCHI KUHUSU UCHAGUZI MKUU UJAO OCTOBA 2010

NAMBA 17

OKTOBA, 2010

1. Utangulizi

Mpango wa Utafiti na Elimu ya Demokrasia (REDET) umekuwa na utaratibu wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu masuala mbalimbali muhimu ya kitaifa ikiwa pamoja na uchaguzi. Kama itakumbukwa hapo mwezi Machi mwaka huu 2010, REDET ilifanya tafiti ya 16 kuhusu maoni ya wananchi kuhusu uchaguzi mkuu ujao wa Oktoba 2010. Kama ilivyokuwa katika tafiti zilizopita, huu ni utafiti wa 17 ambao matokeo yake yanatokana na utafiti uliojumuisha mikoa yote 26 ya Tanzania. Sampuli nasibu (random sampling) ilitumika kuchagua wilaya mbili katika kila mkoa. Jumla ya wahojiwa wote ilikuwa ni 2600, ikiwa ni wahojiwa 50 kutoka katika kila wilaya iliyochaguliwa.

Lengo kuu la utafiti huu ni kuboresha shughuli za serikali kwa kuleta maendeleo kwa watu walio wengi na kuimarisha demokrasia nchini. Inatarajiwa kwamba matokeo haya yatawezesha vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi kuangalia sera na manifesto zao ili ziendane na mahitaji na matakwa ya wananchi. Aidha ni muhimu kufahamu kuwa utafiti huu ulifanyika Septemba 2010. Kwa hiyo basi, matokeo haya yanaonyesha mwelekeo, maoni na tathmini ya wahojiwa katika kipindi hicho. Mambo kadha yanaweza kutokea ambayo yanaweza kubadilisha maoni na mitazamo ya watu hapo ifikapo Oktoba 31, 2010 wakati wa uchaguzi.

2. Mfumo wa Ukusanyaji Maoni

Ukusanyaji wa maoni kwa ajili ya utafiti huu ulifanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Sampuli ilichaguliwa kwa kutumia ngazi tatu (3-level multi-stage sampling). Ngazi hizo ni wilaya, vijiji/mitaa na wahojiwa. Katika kila ngazi sampuli ilipatikana kwa kutumia mtindo wa sampuli nasibu (random sampling method). Wilaya 52 zifuatazo ndizo zilizochaguliwa:

MKOA	**WILAYA**
1. DODOMA	1. Dodoma Urban (U) 2. Chamwino
2. ARUSHA	1. Arusha (U) 2. Monduli
3. KILIMANJARO	1. Moshi Rural 2. Hai
4. TANGA	1. Tanga (U) 2. Handeni
5. MOROGORO	1. Morogoro Urban (U) 2. Mvomero
6. PWANI	1. Bagamoyo 2. Kisarawe
7. DAR ES SALAAM	1. Kinondoni (U) 2. Temeke (U)
8. LINDI	3. Lindi Urban (U) 4. Ruangwa
9. MTWARA	1. Masasi 2. Newala
10. RUVUMA	1. Songea Urban (U) 2. Namtumbo
11. IRINGA	1. Iringa Urban (U) 2. Kilolo
12. MBEYA	1. Mbeya Urban (U) 2. Ileje
13. SINGIDA	1. Iramba 2. Manyoni
14. TABORA	1. Nzega 2. Urambo
15. RUKWA	1. Sumbawanga Urban (U) 2. Nkansi
16. KIGOMA	1. Kigoma Urban (U) 2. Kigoma Rural
17. SHINYANGA	1. Shinyanga Rural 2. Bariadi
18. KAGERA	1. Bukoba Urban (U) 2. Muleba
19. MWANZA	1. Ilemela (U) 2. Sengerema
20. MARA	1. Bunda 2. Serengeti

MKOA	**WILAYA**
21. MANYARA	1. Babati 2. Mbulu
22. NORTH UNGUJA	1. North "A" 2. North "B"
23. SOUTH UNGUJA	1. South 2. Central
24. URBAN WEST	1. Urban (U) 2. West (U)
25. NORTH PEMBA	1. Wete 2. Micheweni
26. SOUTH PEMBA	1. Chake Chake 2. Mkoani

Katika Kila wilaya, watafiti walitakiwa kuchagua vijiji viwili (kwa maeneo ya shamba) au mitaa miwili (kwa maeneo ya mjini) kwa kutumia njia ya sampuli nasibu (random selection). Katika kila wilaya, jumla ya wahojiwa 50 walichaguliwa, 25 kutoka katika kila kijiji/mtaa. Kati ya wahojiwa 50 katika kila wilaya, 25 walitakiwa wawe wanawake na wengine 25 wawe wanaume. Uchaguzi wote wa wahojiwa ulifanyika kwa kutumia njia ya sampuli nasibu (random selection).

Sampuli iliyochaguliwa ilizingatia mgawanyo wa idadi ya watu waishio mijini na vijijini hapa nchini. Hivyo basi, asilimia 70 ya vijiji/mitaa ilichaguliwa kutoka katika mazingira ya shamba na asilimia 30 kutoka katika mazingira ya mjini. Watafiti wakuu (Principal Researchers) walisimamia zoezi zima la utafiti huu lililoendeshwa na watafiti wasaidizi (research assistants) 52. Watafiti wakuu na watafiti wasaidizi walipewa mafunzo ya pamoja jinsi ya kuuliza maswali kwa wahojiwa, kupata sampuli nasibu na maadili ya mtafiti.

Ili kuweza kulinganisha matokeo ya tafiti za huko nyuma, maswali yale yale yaliulizwa tena katika utafiti huu. Swali kuu la msingi katika utafiti huu lilikuwa: Kama uchaguzi mkuu ungefanyika leo (Septemba 2010), je wahojiwa wangemchagua mgombea wa

chama gani?. Maswali mengine yanayopima kiwango cha uridhishwaji wa utendaji kazi wa vyama vya siasa yaliuliza wahojiwa kutoa maoni yao kama 'wanaridhika sana', 'wanaridhika kiasi' au 'hawaridhiki'.

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu kuu sita. Tukianzia na sehemu ya utangulizi na mfumo wa ukusanyaji maoni hapo juu, sehemu ya pili inawasilisha maoni ya wananchi kuhusu uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani. Sehemu ya tatu inawasilisha tathmini ya wananchi kuhusu utendaji kazi wa vyama vya siasa katika masuala mbalimbali. Sehemu ya nne inawasilisha matokeo ya utafiti kuhusu vyombo vya habari. Sehemu ya tano ni masuala mengineyo ikifuatiwa na sehemu ya mwisho ambayo inatoa hitimisho.

3. Matokeo

3.1 Maoni ya Watu kuhusu Vyama vya siasa na Wagombea

Wahojiwa walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani. Swali liliulizwa kama ifuatavyo "*Mwezi Oktoba mwaka huu utafanyika uchaguzi mkuu. Kama uchaguzi huo ungefanyika leo, je wewe ungemchagua mgombea wa chama gani*?" Jedwali 1 linawasilisha matokeo hayo. Tukianzia na uchaguzi wa Rais wa serikali ya muungano, asilimia 71.2 ya wahojiwa wote walisema wao watamchagua mgombea wa urais wa CCM. Ilifuatiwa na CHADEMA ambapo asilimia 12.3 walisema watamchagua mgombea wa CHADEMA, na asilimia 10.1 walisema watamchagua mgombea wa CUF. Vyama vingine vilipata idadi ndogo sana ya wahojiwa kama jedwali namba 1 linavyoonyesha. Asilimia 5.6 walisema bado hawajaamua ni mgombea wa chama gani watampigia kura.

Kwa upande wa uchaguzi wa wabunge wa Jamhuri ya Muungano, asilimia 66.7 ya wahojiwa wote walisema watamchagua mgombea wa CCM, asilimia 11.7 watamchagua mgombea wa CUF na asilimia 11.5 watamchagua mgombea wa CHADEMA. Vyama vingine vinatajwa na idadi ndogo sana ya wahojiwa.

Katika uchaguzi wa madiwani, asilimia 66 walisema watamchagua mgombea wa CCM, asilimia 11.5 watamchagua mgombea wa CUF na asilimia 10.3 walisema watamchagua mgombea wa CHADEMA. Baadhi ya wahojiwa walisema bado hawajaamua ni chama gani cha kukipigia kura katika uchaguzi wa wabunge (7.8%) na madiwani (10.4%).

Jedwali 1: Maoni ya Watu Kuhusu Vyama vya Siasa na Wagombea (Asilimia na Idadi ya wahojiwa kwenye mabano)

Chama cha Siasa	**Rais**	**Wabunge**	**Madiwani**
CCM	71.2 (1849)	66.7 (1733)	66.0 (1715)
CUF	10.1 (263)	11.7 (304)	11.5 (298)
CHADEMA	12.3 (319)	11.5 (299)	10.3 (268)
TLP	0.4 (11)	1.0 (25)	0.7 (18)
NCCR-M	0.3 (8)	1.1 (28)	1.0 (26)
CCJ	-	-	0.0 (1)
UDP	0.0 (1)	0.0 (1)	0.1 (2)
Jahazi Asilia	-	-	0.0 (1)
DEMOKRASIA MAKINI	0.0 (1)	0.0 (1)	0.0 (1)
AFP		0.1 (2)	-
UPDP	0.0 (1)	-	-
Sijaamua bado	5.6 (146)	7.8 (204)	10.4 (269)
Jumla	**100 (2598)**	**100 (2598)**	**100 (2599)**

Matokeo haya yanaonyesha mambo kadhaa;

Kwanza, mgombea urais wa CCM anaonekana kupata kura nyingi zaidi (71.2%) kuliko kura za wabunge wa CCM (66.7%) na madiwani wa CCM (66%). Kwa mfano, kiwango cha kura za wabunge kinapungua kwa asilimia 4.5 ukilinganisha na kile cha kura za urais. Pili, mgombea urais wa CHADEMA anaonekana kupata kura nyingi kiasi (12.3%) kuliko kura za wabunge wa CHADEMA (11.5%) na madiwani wake (10.3%). Kwa upande wa CUF, kura za wabunge (11.7%) na madiwani (11.5%) ziko juu kidogo ukilinganisha na zile za urais (10.1). Tatu, ukiachilia mbali CUF na CHADEMA, vyama vingine vya upinzani vina idadi finyu sana ya wahojiwa wanaosema wangevipigia kura kama uchaguzi ungefanyika Septemba 2010. Nne, kuna idadi ya wahojiwa ambayo bado haijafanya maamuzi ni mgombea wa chama gani wa kumpigia kura. Idadi ni kubwa zaidi kwa uchaguzi wa madiwani (10.4%) na wabunge (7.8%) kuliko wa urais (5.6%) (Jedwali namba 1)

Tano, itakumbukukwa kwamba matokeo ya utafiti wa REDET wa hapo Machi mwaka huu 2010, yalionyesha wahojiwa wengi walisema wangechagua mgombea urais wa CCM (77.2%), wabunge (68%) na madiwani (68.2%). Katika utafiti huu wa Septemba, bado CCM inaongoza. Hata hivyo, kiwango cha asilimia za kura imepungua kama Jedwali namba 2, 3 na 4 yanavyoonyesha. Kwa upande wa uchaguzi wa urais, wakati asilimia 77.2 ya wahojiwa wote walisema wangechagua mgombea urais wa CCM kama uchaguzi ungefanyika hapo Machi mwaka huu, ni asilimia 71.2 ndio wamesema hivyo hapo Septemba 2010. Yaani, katika kipindi cha miezi sita, idadi ya wahojiwa wanaosema watamchagua mgombea urais wa CCM imepungua kwa asilimia 6.

Jedwali 2: Mgombea Urais: Mlinganisho na Utafiti wa REDET wa Machi 2010 na Septemba 2010

Chama cha Siasa	Utafiti		Tofauti (-/+)
	March	Sept	
CCM	77.2	71.2	-6
CUF	9.2	10.1	+0.9
CHADEMA	4.2	12.3	+8.1
TLP	0.2	0.4	+0.2
NCCR-M	0.2	0.3	+0.1
UDP	-	-	-
CHAUSTA	0.1	-	-0.1

Aidha, Jedwali namba 2 linaonyesha kwamba vyama vinne vya upinzani vikiongozwa na CHADEMA vimeweza kujiongezea idadi ya kura. Ukilinganisha vyama vyote, ni mgombea wa Urais wa CHADEMA ndio ameongeza idadi ya kura kwa kiwango kikubwa. Wakati asilimia 4.2 tu ya wahojiwa wote walisema wangechagua mgombea urais wa CHADEMA kama uchaguzi ungefanyika hapo Machi mwaka huu, ni asilimia 12.3 wamesema hivyo hapo Septemba 2010. Yaani, katika kipindi cha miezi sita, idadi ya wahojiwa wanaosema watamchagua mgombea urais wa CHADEMA imeongezeka kwa asilimia 8. Kwa upande wa CUF, kiwango cha kura kimeongezeka kwa asilimia 0.9 tu. Aidha, TLP imeweza kuongeza kiwango cha kura kutoka asilimia 0.2 kwenda asilimia 0.4 na NCCR-M imepanda kidogo kutoka asilimia 0.2 hadi asilimia 0.3. Mabadiliko haya yanaonekana kujitokeza kutokana na kampeni za uchaguzi zinazoendelea hivi sasa. Aidha, hapo Machi 2010, vyama vilikuwa havijatangaza rasmi wagombea urais wao na Tume ya Uchaguzi ilikuwa bado haijapitisha majina wa wagombea.

Jedwali 3: Mgombea Ubunge: Mlinganisho wa Utafiti wa REDET wa Machi 2010 na Septemba 2010

Chama cha Siasa	Utafiti		Tofauti
	March	Sept	-/+
CCM	68.0	66.7	-1.3
CUF	10.2	11.7	+1.5
CHADEMA	8.6	11.5	+2.9
TLP	0.2	1.0	+0.8
NCCR-M	0.3	1.1	+0.8
UDP	0.1	0.0	-0.1

Kwa upande wa wabunge, wakati asilimia 68 ya wahojiwa wote walisema wangechagua mgombea ubunge wa CCM kama uchaguzi ungefanyika hapo Machi mwaka huu, ni asilimia 66.7 ndio wamesema hivyo hapo Septemba 2010. Yaani, katika kipindi cha miezi sita, idadi ya wahojiwa wanaosema watamchagua mgombea ubunge wa CCM imepungua kidogo kwa asilimia 1.3, na kwa upande wa CHADEMA wameongezeka kwa asilimia 2.9, CUF kwa asilimia 1.5, TLP kwa asilimia 0.8 na NCCR-M kwa asilimia 0.8.

Jedwali 5: Mgombea Udiwani: Mlinganisho na Utafiti wa REDET wa Machi 2010 na Septemba 2010

Chama cha Siasa	Utafiti		Tofauti
	March	Sept	-/+
CCM	68.2	66.0	-2.2
CUF	10.6	11.5	+0.9
CHADEMA	7.7	10.3	+2.6
TLP	0.2	0.7	+0.5
NCCR-M	0.2	1.0	+0.8
UDP	0.1	0.1	0.0

Aidha, matokeo hayo yanaonyesha kujirudia katika maoni ya wahojiwa kuhusu wagombea udiwani. Wakati asilimia 68.2 ya wahojiwa wote walisema wangechagua mgombea udiwani wa CCM kama uchaguzi ungefanyika hapo Machi mwaka huu, ni asilimia 66 ndio wamesema hivyo hapo Septemba 2010, na hivyo kufanya pungufu ya asilimia 2.2. Kwa upande wa CHADEMA, idadi hii ya wahojiwa imeongezeka kwa asilimia 2.6, CUF kwa asilimia 0.9, TLP kwa asilimia 0.5 na NCCR-M kwa asilimia 0.8.

3.2 Jina la Mgombea Urais na Sifa Zake

Kuhusu uchaguzi wa rais wa serikali ya Jamhuri ya Muungano, wahojiwa waliulizwa kutaja jina la mtu mmoja ambaye wangependa kumchagua ili awe rais wa Tanzania. Rais Jakaya Mrisho Kikwete anaongoza kwa kutajwa na asilimia 68.5 ya wahojiwa wote, akifuatiwa na Dr. Wilbrod Slaa ambaye anatajwa na asilimia na 11.9. Nafasi ya tatu inashikiliwa na Prof. Ibrahim Lipumpa ambaye anatajwa na asilimia 9.3 ya wahojiwa.

Majina mengine yaliyotajwa na asilimia ndogo sana ya wahojiwa kama Jedwali namba 6 linavyoonyesha.

Jedwali 6: Maoni ya Watu kuhusu Mgombea Urais

Jina	**Idadi ya Wahojiwa**	**Asilimia (%)**
Mh. Jakaya Mrisho Kikwete (CCM)	1779	68.5
Mh. Wilbrod Slaa (CHADEMA)	309	11.9
Prof. Ibrahim Lipumba (CUF)	242	9.3
Mh. Mugahywa Mutamwega (TLP)	11	0.4
Mh. Rungwe Hashim (NCCR-M)	3	0.1
Bado sijaamua	224	8.7
Mengineyo	28	1.1
Jumla	**2597**	**100**

Wahojiwa waliulizwa kutaja sifa moja kubwa ambayo itawafanya wampigie kura mgombea fulani wa Urais (Jedwali no. 6). Mgombea mwenye uzoefu katika uongozi ndio ilikuwa sifa ya kwanza iliyotajwa na asilimia 14.8 ya wahojiwa wote. Sifa ya pili ilikuwa ni mgombea anayejali wanyonge/maskini iliyotajwa na asilimia 14.1. Sifa nyingine ni mgombea wa chama changu (12.5%), mgombea mwadilifu asiyeshiriki rushwa/ufisadi (9.9%), na mgombea mwenye elimu kubwa (1.9%) (Jedwali namba 7)

Jedwali 7 : Sifa za Mgombea Urais Unayemtaka

Sifa za Mgombea	**Asilimia na Idadi kwenye mabano**
Mwenye uzoefu katika Uongozi	14.8 (383)
Anayejali wanyonge/maskini	14.1 (365)
Mgombea wa chama changu	12.5 (323)
Asiyeshiriki rushwa/asiye fisadi	9.9 (258)
Mwenye elimu kubwa	1.9 (49)
Bado hajaamua	4.2 (108)
Mengineyo	35.8 (931)
Sijui	6.8 (176)
Jumla	**100** **(2593)**

3.3 Uchambuzi Katika Wilaya wa Maoni ya Wananchi Kuhusu Uchaguzi wa Urais na Wabunge kwa Vyama Vikuu Vitatu (CCM, CHADEMA na CUF)

Uchambuzi zaidi katika ngazi ya wilaya ya maoni ya wananchi kuhusu chama watakachopigia kura kwa mgombea Urais na wabunge yanaashiria yafuatayo (Jedwali Namba. 7);

Kwanza, mgombea urais wa CCM anatajwa kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 katika kila wilaya 43 zilizofanyiwa utafiti huu[1]. Katika wilaya 9 mgombea urais wa CCM anatajwa na idadi chini ya asilimia 50. Hizi ni Arusha mjini (48%), Kinondoni (24%), Kigoma Mjini (48%), Kigoma vijijini (28%), Babati (40%), Mvomero (44%), Ilemela (48%), Micheweni (44%), Mkoani (32%).

Pili, mgombea urais wa CHADEMA anatajwa kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 katika kila wilaya 3 nazo ni Kinondoni (64%), Kigoma vijijini (56%), na Babati (58%). Aidha, mgombea urais wa CHADEMA anaonekana kuungwa mkono katika wilaya ya Arusha mjini (40%), Iringa mjini (20%), Bukoba mjini (26%), Kigoma mjini (32%), Mbulu (36%), Serengeti (20%), Ileje (34%), Mvomero (44%) na Ilemela mjini (36%).

Tatu, mgombea urais wa chama cha CUF anatajwa kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 katika kila wilaya 1 nayo ni Mkoani (68%). Kwa ujumla mgombea urais wa CUF anaonekana kuungwa mkono katika wilaya za Wete (36%), Chakechake (30%), Micheweni (44%), Magharibi (48%), Kaskazini Unguja (32%), Tanga mjini (22%), Shinyanga vijijini (34%), Newala (28%) na Lindi mjini (16%).

[1] Katika utafiti wa REDET uliofanyika hapo Machi mwaka huu mgombea urais wa CCM alitajwa kuchaguliwa na zaidi ya asilimia 50 katika kila wilaya 50 zilizofanyiwa utafiti huu[1]. Ni wilaya 2 tu ambazo mgombea wa CCM alitajwa na idadi chini ya asilimia 50. Hizi ni Wete (40%) na Tandahimba (42%).

Jedwali 8: Maoni ya Wananchi Kuhusu Uchaguzi wa Rais na Wabunge Kwa Wilaya

Wilaya	Uchaguzi wa Urais			Uchaguzi wa Wabunge		
	CCM	CHADEMA	CUF	CCM	CHADEMA	CUF
Arusha mjini	48.0	40.0	8.0	60.0	30.0	6.0
Monduli	82.0	8.0	-	88.0	4.0	-
Kinondoni	24.0	64.0	8.0	28.0	60.0	4.0
Temeke	70.0	2.0	16.0	66.0	2.0	18.0
Dodoma mjini	84.0	12.0	-	76.0	16.0	-
Chamwino	80.0	12.0	6.0	88.0	6.0	4.0
Iringa mjini	70.0	20.0	8.0	60.0	30.0	8.0
Kilolo	88.0	-	-	86.0	-	-
Bukoba mjini	74.0	26.0	-	84.0	14.0	-
Muleba	82.0	14.0	-	84.0	12.0	-
Kigoma mjini	48.0	32.0	8.0	42.0	32.0	10.0
Kigoma vijijini	28.0	56.0	4.0	20.0	58.0	6.0
Moshi vijijini	88.0	-	-	32.0	-	-
Hai	90.0	10.0	-	60.0	34.0	-
Lindi mjini	70.0	6.0	16.0	50.0	-	36.0
Ruangwa	80.0	2.0	12.0	80.0	-	14.0
Babati	40.0	58.0	-	42.0	18.0	-
Mbulu	60.0	36.0	-	74.0	12.0	-
Bunda	64.0	14.0	-	56.0	16.0	4.0
Serengeti	58.0	20.0	4.0	58.0	24.0	6.0
Mbeya mjini	84.0	12.0	2.0	84.0	12.0	2.0
Ileje	52.0	34.0	6.0	60.0	20.0	10.0

Morogoro mjini	61.2	4.1	12.2	58.0	4.0	16.0
Mvomero	44.0	44.0	-	36.0	50.0	2.0
Masasi	82.0	8.0	8.0	76.0	4.0	14.0
Newala	66.0	-	28.0	64.0	2.0	26.0
Ilemela mjini	48.0	36.0	6.0	42.0	34.0	4.0
Sengerema	90.0	10.0	-	96.0	4.0	-
Bagamoyo	86.0	-	4.0	86.0	2.0	2.0
Kisarawe	84.0	-	14.0	84.0	-	14.0
Sumbawanga mjini	84.0	6.0	-	46.0	38.0	-
Nkasi	100.0	-	-	100.0	-	-
Songea mjini	90.0	10.0	-	82.0	16.0	-
Namtumbo	78.0	6.0	8.0	80.0	2.0	6.0
Shinyanga vijijini	62.0	2.0	34.0	58.0	2.0	38.0
Bariadi	77.6	6.1	6.1	77.6	4.1	4.1
Iramba	96.0	2.0	2.0	96.0	2.0	2.0
Manyoni	90.0	8.0	2.0	82.0	14.0	4.0
Nzega	86.0	12.0	-	68.0	8.0	12.0
Urambo	94.0	-	6.0	94.0	2.0	2.0
Tanga mjini	56.0	2.0	22.0	44.0	4.0	32.0
Handeni	96.0	-	2.0	94.0	-	2.0
North”A”	68.0	-	32.0	62.0	-	38.0
North”B”	92.0	2.0	6.0	92.0	2.0	6.0
Kusini	92.0	-	6.0	92.0	-	6.0
Kati	96.0	-	-	94.0	-	-

Mjini	80.0	2.0	4.0	80.0	-	4.0
Magharibi	50.0	-	48.0	50.0	-	48.0
Wete	54.0	-	36.0	48.0	2.0	42.0
Micheweni	44.0	-	44.0	38.8	-	49.0
Chake chake	58.0	-	30.0	52.0	2.0	28.0
Mkoani	32.0	-	68.0	18.0	-	80.0
Jumla	**71.2 (1849)**	**12.3 (319)**	**10.1 (263)**	**66.7 (1733)**	**11.5 (299)**	**11.7 (304)**

Nne, tukichambua maoni ya wahojiwa kuhusu uchaguzi wa wabunge, inaonekana kwamba CCM inaungwa mkono zaidi ya asilimia 50 katika wilaya 40 zilizofanyiwa utafiti huu. Hata hivyo, CCM inaonekana kupata upinzani katika katika wilaya zifuatavyo; Kinondoni (28%), Kigoma mjini (42%), Kigoma vijijini (20%), Moshi vijijini (32%), Lindi Mjini (50%), Babati (42%), Mvomero (36%), Ilemela (42%), Tanga mjini (44%), Mjini Unguja (50%), Wete (48%), Micheweni (38.8%), na Mkoani (18%).

Tano, wagombea ubunge wa CHADEMA wanaonekana kuungwa mkono Kinondoni (60%), Kigoma vijijini (58%), Mvomero (50%), Sumbawanga mjini (38%), Ilemela mjini (34%), Kigoma mjini (32%), Hai (34%), Serengeti (20%), Ileje (20%), Arusha mjini (30%) na Iringa mjini (30%).

Sita, wagombea ubunge wa CUF wanaonekana kuungwa mkono katika wilaya ya Lindi mjini (36%), Newala (26%), Shinyanga vijijini (38%), Tanga mjini (32%), Kaskazini A (38%), Magharibi (48%), Wete (42%), Micheweni (49%) na Mkoani (80%).

Saba, kwa ujumla, vyama vingine kama NCCR-M na TLP vinaungwa mkono na kiwango kidogo sana cha wahojiwa. Hata hivyo kuna sehemu chache ambazo vyama hivi vinatajwa kama chaguo la wahojiwa. Kwa upande wa uchaguzi wa wabunge, NCCR-M

inatajwa katika wilaya za Babati (30%), Kinondoni (6%) na Moshi vijijini (6%). TLP inatajwa Moshi vijijini (30%) na Bunda (10%).

3.4 Maoni ya Wahojiwa Kuhusu Kero/Tatizo Kuu

Wahojiwa waliulizwa kutaja tatizo moja kubwa ambalo wanaliona kwamba serikali itakayoingia madarakani ilipe kipaumbele. Kama jedwali namba 9 linavyoonyesha, suala linaloongoza ni elimu ambalo linatajwa na asilimia 28.3 ya wahojiwa wote. Suala la pili ni kilimo (13.4%), likifuatiwa na huduma za afya (11.2%). Suala la nne ni maji (9.4%), likifuatiwa na barabara (7.1%), ajira (4.8%), amani na umoja (2.9%), mikopo na mitaji (2.3%), kupambana na rushwa (2.0%) na mengineyo kama yanavyoonekana katika jedwali no. 9.

Jedwali 9: Suala/Tatizo Kubwa kwa Wananchi Serikali Ijayo Ilizingatie

Tatizo	**Asilimia na Idadi**
Elimu	28.3 (734)
Kilimo	13.4 (348)
Afya	11.2 (290)
Maji	9.4 (245)
Barabara	7.1 (184)
Ajira	4.8 (126)
Amani na umoja	2.9 (76)

Mikopo na mitaji	2.3 (59)
Kupambana na rushwa	2.0 (51)
Umeme	1.5 (39)
Muungano	1.1 (29)
Viwanda	1.1 (29)
Sijui	1.1 (26)
Mengineyo	13.8 (358)
Jumla	**100** **(2598)**

4.0 Utendaji Kazi wa Vyama vya Siasa

Wahojiwa waliulizwa kutoa tathmini yao kuhusu utendaji kazi wa chama tawala, CCM, na vyama vya upinzani kwa ujumla wake katika mfumo huu wa vyama vingi. Kwa upande wa utendaji kazi wa CCM, asilimia 57.4 walisema wanaridhika sana na utendaji kazi wake. Wale waliosema wanaridhika kiasi ni asilimia 20.7, asilimia 12.3 walisema wao hawaridhiki na asilimia 7 walisema hawaridhiki kabisa (Jedwali namba 10)

Kwa upande wa utendaji kazi wa vyama vya upinzani, asilimia 35.6 ya wahojiwa wote walisema wanaridhika sana na utendaji kazi wa vyama vya upinzani wakati asilimia 22.6 wanaridhika kiasi, asilimia 23 ya wahojiwa wote walisema hawaridhiki na asilimia 7.2 walisema hawaridhiki kabisa.

Jedwali 10: Tathmini ya Utendaji Kazi wa Vyama vya Siasa

Kiwango	**CCM**	**Vyama vya Upinzani**
Naridhika sana	57.4 (1493)	35.6 (923)
Naridhika kiasi	20.7 (537)	22.6 (587)
Siridhiki	12.3 (319)	23.0 (596)
Siridhiki kabisa	7.0 (182)	7.2 (188)
Mengineyo	2.7 (68)	11.6 (301)
Jumla	**100 (2599)**	**100 (2595)**

Tukilinganisha matokeo haya na yale ya Utafiti wa Machi wa REDET inaonyesha mambo kadhaa. Kiwango cha uridhishwaji na utendaji kazi wa chama tawala katika mfumo wa vyama vingi unaonekana kuongezeka. Wakati asilimia 48.3 walisema wanaridhika sana hapo Machi 2010, kiwango hicho kimeongezeka na kufikia asilimia 57.4 hapo Septemba mwaka huu (Jedwali 11).

Jedwali 11: Tathmini ya Utendaji Kazi wa Vyama vya Siasa

	CCM		**Vyama vya Upinzani**	
Kiwango	**Machi**	**Sept**	**Machi**	**Sept**
Naridhika sana	48.3	57.4	20.5	35.6
Naridhika kiasi	35.7	20.7	28.7	22.6
Siridhiki	14.8	12.3	44.4	23.0
Siridhiki kabisa	-	7.0	-	7.2
mengineyo	1.1	2.7	6.4	11.6
Jumla	**100**	**100**	**100**	**100**

Ukiangalia kwa upande wa upinzani, ukilinganisha matokeo ya Machi na Septemba 2010, idadi ya wahojiwa wanaosema wanaridhika sana na utendaji kazi wa vyama vya upinzani inaonekana kuongezeka kutoka asilimia 20.5 hapo Machi na kufikia asilimia 35.6 hapo Septemba mwaka huu.

Sababu za Kuridhika kiasi au kutokuridhika na utendaji wa vyama vya siasa

Aidha, wahojiwa waliulizwa kutaja sababu za 'kuridhika kiasi' au 'kutokuridhika' na utendaji kazi wa chama tawala. Sababu zifuatavyo zilitajwa; hakitimizi ahadi (12.7%), viongozi wake ni wala rushwa (7.7%), viongozi wake hawaaminiki (4.3%), hakina sera/program nzuri (1.3%), kina migogoro (2.8%), n.k. (jedwali namba 12)

Jedwali 12: Sababu za Kuridhika Kiasi au Kutokuridhika na Utendaji Kazi wa Chama Tawala (CCM)

Sababu	**Asilimia na Idadi**
Hakitimizi ahadi zake	12.9 (333)
Viongozi wake ni wala rushwa	7.7 (198)
Viongozi wake hawaaminiki/wabovu	4.3 (111)
Hakina sera/program nzuri	1.3 (34)
Kina migogoro	2.8 (72)
Hakina uwezo wa kuongoza nchi	0.7 (18)
Sijui	12.0 (308)
Hawahusiki (walisema wameridhika sana na mengieyo)	58.3 (1504)
Jumla	**100** **(2580)**

Hali kadhalika, wahojiwa waliulizwa kutaja sababu za 'kuridhika kiasi' au 'kutokuridhika' na utendaji kazi wa vyama vya upinzani. Sababu zifuatavyo zilitajwa; viongozi wake hawaaminiki (7.6%), havina sera (6.5%), vina migogoro (6.2%), havina uwezo wa kuongoza nchi (5.3%), n.k. (jedwali namba 13)

Jedwali 13: Sababu za Kuridhika Kiasi au Kutokuridhika kabisa na Utendaji Kazi wa Vyama vya Upinzani

Sababu	**Asilimia na Idadi**
Viongozi wake hawaaminiki	7.6 (196)
Havina sera/programu nzuri	6.5 (169)
Vina migogoro	6.2 (160)
Havina uwezo wa kuongoza nchi	5.3 (137)
Vimeshindwa Kuiwajibisha serikali	1.4 (35)
Sijui	30.1 (778)
Hawausiki (karidhika sana na Mengineyo	42.9 (1104)
Jumla	**100** **(2582)**

5.0 Tathmini ya Vyombo vya Habari

Wahojiwa waliulizwa kutaja chanzo kimoja kikubwa cha habari za kampeni za uchaguzi hapo Oktoba 2010. Asilimia 62.3 ya wahojiwa wote walitaja radio kama chanzo chao kikuu cha habari za kampeni, asilimia 19.7 walitaja televisheni na asilimia 4.0 walitaja magazeti (Jedwali 14). Asilimia 4.3 ya wahojiwa wote walisema wao hawafuatilii kampeni za uchaguzi.

Jedwali 14: Chanzo kikubwa cha habari za kampeni za uchaguzi

Chanzo cha habari	**Asilimia na Idadi kwenye mabano**
Radio	62.4 (1620)
Televisheni	19.7 (511)
Magazeti	4.0 (105)
Sifuatilii kampeni	4.3 (112)
Mengineyo	9.5 (248)
Jumla	**100** **(2596)**

Aidha, wahojiwa waliulizwa kufanya tathmini na kutoa maoni yao kama vyombo vya habari vinatoa haki sawa kwa vyama vyote katika kutoa taarifa za kampeni. Asilimia 59.9 walisema ndiyo, vyombo vya habari vinatoa haki sawa kwa vyama vyote vya siasa, asilimia 19.4 walisema hapana, vinapendelea chama tawala, na asilimia 1 walisema vinapendelea vyama vya upinzani (Jedwali 15).

Jedwali 15: Vyombo vya habari vinatenda haki?

Maoni	**Asilimia na Idadi**
Ndiyo, vinatenda haki sawa kwa vyama vyote	59.9 (1553)
Hapana, vinapendelea chama tawala	19.4 (504)
Hapana, vinapendelea upinzani	1.0 (26)
Havitoi taarifa kuhusu kampeni za vyama	0.7 (18)
Mengineyo	19.0 (493)
Jumla	**100** **(2592)**

Wahojiwa waliulizwa kutaja chanzo kingine cha habari za kampeni za uchaguzi. Kama jedwali namba 16 linavyoonyesha, mikutano ya hadhara inaongoza kwa kutajwa na asilimia 38 ya wahojiwa wote, wakifuatiwa ndugu na marafiki (21%), chama changu cha siasa (6%), mabango na vipeperushi (4%). Ingawa vinatajwa na asilimia ndogo sana, makanisa (0.6%) na misikiti (0.3%) nayo yanatajwa kama chanzo cha habari za kampeni kwa baadhi ya watu.

Jedwali 16: Chanzo kingine cha habari za kampeni za uchaguzi

Chanzo cha habari	Asilimia na Idadi kwenye mabano
Mikutano ya Hadhara	38.1 (982)
Ndugu na marafiki	21.1 (543)
Chama changu cha siasa	6.1 (156)
Mabango na vipeperushi	4.0 (103)
Kanisani	0.6 (16)
Msikitini	0.3 (9)
Internet	0.3 (9)
Sifuatilii kampeni	4.7 (122)
Mengineyo	24.7 (635)
Jumla	100 (2575)

6.0 Masuala Mengineyo

6.1 Maoni ya Wananchi kuhusu Kuchangia Vyama vya Siasa

Katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi ambapo fedha zinatumika na vyama na wagombea, wahojiwa waliulizwa kama wanachangia fedha vyama vya siasa ili kuviwezesha kufanya shughuli zake za kampeni. Ni asilimia 13.3 tu ya wahojiwa wote walisema wao wanachangia. Idadi kubwa ya wahojiwa, yaani asilimia 83.8 walisema hawachangii. Suala la kujiuliza je, ni wapi vyama na wagombea wanapata fedha za kampeni!

Jedwali 17: Kuchangia Vyama Vya Siasa Katika Uchaguzi

Maoni	**Asilimia na Idadi**
Ndiyo, nachangia	13.3 (346)
Hapana, sichangii	83.8 (2174)
Mengineyo	2.8 (73)
Jumla	**100** **(2593)**

Wahojiwa waliulizwa kutoa tathmini yao kama wameridhika au la kwa jinsi vyama vya siasa vilivyoendesha mchakato wa kuchagua wagombea wao ndani ya vyama. Asilimia 54.6 walisema wameridhika sana na jinsi zoenzi hilo lilivyoendeshwa ndani ya vyama. Aidha, asilimia 14.9 walisema wameridhika kiasi, asilimia 12.4 walisema hawajaridhika na asilimia 4.6 walisema hawakuridhika kabisa (Jedwali 18)

Jedwali 18: Tathmini ya Wahojiwa Kuhusu Uchaguzi wa Wagombea ndani ya Vyama vya Siasa

Kiwango cha Kuridhika	**Asilimia na Idadi kwenye mabano**
Naridhika sana	54.6 (1417)
Naridhika kiasi	14.9 (386)
Siridhiki	12.4 (321)
Siridhiki Kabisa	4.6

	(119)
Mengineyo	13.6 (30)
Jumla	**100** **(2596)**

9.0 Majumuisho

Matokeo ya utafiti huu yanaashiria kwamba endapo uchaguzi ungefanyika hapo Septemba 2010, CCM ingeweza kushinda katika uchaguzi wa urais, wabunge na madiwani. Hata hivyo, baada ya takribani mwezi mmoja wa kampeni za uchaguzi, kiwango cha uungwaji mkono cha CCM kinapungua wakati kile cha vyama vya upinzani hasa CHADEMA na CUF kinaongezeka. Wananchi walio wengi wanategemea radio kama chanzo chao kikuu cha kupata taarifa za kampeni za vyama na wagombea. Aidha, wahojiwa wengi wana maoni kwamba vyombo vya habari vinajitahidi kutoa nafasi sawa kwa vyama vyote vya siasa. Pia, elimu ni suala la kwanza ambalo wahojiwa wanataka serikali ijayo ilipe kipaumbele likifuatiwa na kilimo, Afya na maji. Mwisho, ni muhimu kutambua kwamba, matokeo haya ya utafiti huu wa 17 wa REDET yanaonyesha maoni ya wananchi katika kipindi kile ambacho utafiti ulifanywa, yaani mwezi wa tisa mwaka huu. Katika kipindi kilichobaki kuelekea uchaguzi, mambo kadhaa yanaweza kutokea ambayo yanaweza kubadilisha mwelekeo na mtazamo wa wapiga kura.